# Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Muktadha wa Utandawazi

*Samuel M. Obuchi[1] na Phillip F. O. Ochoi[2]*
[1]*Chuo Kikuu cha Moi*
[2]*Shirika la Uchapishaji la Jomo Kenyatta Foundation*

**Ikisiri**

**Makala haya yanatalii masuala mbalimbali yanayohusu Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika katika ulimwengu na malimwengu ya utandawazi. Kwa muda mrefu, wataalamu wengi wa masuala ya lugha na isimu wamekuwa mbioni katika kuuangazia uhusiano uliopo au unaopaswa kuwepo baina ya lugha na shughuli za kimsingi na maendeleo ya jamii. Mjadala huu hasa umekitwa kwenye mawazo na mikabala ambayo inahusiana moja kwa moja na nguvu na taratibu za utandawazi, ambapo inaaminika kwamba lugha zozote zile ambazo hazitumiwi katika shughuli na harakati za uzalishaji mali huenda zikamezwa na kusahauliwa kabisa hivi karibuni na utamaduni wa Kimagharibi ambao unajitokeza waziwazi katika harakati anuwai za kijamii kama vile uchumi, elimu, uvumbuzi na ugunduzi wa sayansi na teknolojia. Makala haya basi yanaonyesha namna Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika zinaweza kulindwa na kuhifadhiwa ili ziendelee kutumiwa na walio wengi katika shughuli zao za kila siku.**

**Maneno Muhimu:** *Lugha, Utandawazi, Kiswahili, Isimu*

## Utangulizi

Makala haya yanashughulikia nafasi ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika chini ya mfumo wa utandawazi ambao huenda ukachangia pakubwa katika kuzitokomeza kabisa, kwa sababu hazitumiwi kwenye mawasi1iano mapana yanayoumana na utandawazi na mtandao. Baadhi ya maswali yanayoulizwa ni: Je, lugha hizi za Kiafrika zitaweza kuhimili na kuchukuana na usasa na utandawazi? Je, Kiswahili kina nafasi gani katika muktadha huu wa utandawazi? Je, ni hatua gani za kimaksudi zitachukuliwa katika kuzipa hadhi lugha za Kiafrika, kikiwemo Kiswahili? Maswali haya, miongoni mwa mengine, yatamulikwa katika makala haya.

## Lugha za Kiafrika zimo Matumizini

Ukweli usiopingika na ambao utajitokeza dhahiri katika makala haya ni kwamba Kiswahili na baadhi ya lugha za Kiafrika kama vile Kihausa na Kishinyanja ndizo zilizosambaa na kutumiwa na wengi barani Afrika. Kiswahili, kwa mfano,

kinatumiwa kotekote Afrika kama Lingua Franka, yaani lugha ya mawasiliano mapana hasa katika harakati muhimu za wanajamii. Lugha hii imetumiwa kwa muda mrefu sambamba na lugha "tukufu" za kigeni, mathalan, Kijerumani, Kiingereza na Kifaransa.

Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika zimetumiwa kotekote barani, zikitanguliwa na Kiarabu, hasa katika maeneo mbalimbali ya magharibi na kaskazini mwa Afrika. Inaeleweka kwamba Kiarabu ni lugha inayotumiwa na wanajamii wengi, hasa inapokumbukwa kwamba inahusishwa pakubwa na dini na utamaduni wa Kiarabu. Kwa hakika, Kiarabu barani Afrika kinasemwa katika mataifa takribani kumi, na hivyo kukifanya lugha inayosemwa na wengi Afrika ikifuatwa na Kiswahili. Watu wengi nchini Tanzania na Kenya hutumia lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya mama. Ni kutokana na ukweli huu ambapo Kiswahili kimetambuliwa na kufanywa lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya. Hivi ni kusema, Kiswahili na Kiingereza zimetambuliwa kama lugha rasmi, ambapo zinatarajiwa kutumiwa sambamba katika shughuli na harakati rasmi, hususan katika bunge, elimu, biashara na kwenye nyaraka na stakabadhi zilizo rasmi.

Hapa Afrika Mashariki, Kiswahili na lugha za Kiafrika zimejitokeza kama vyombo maridhawa vya mawasiliano kati na baina ya wanajamii wengi (Senanu & Williams, 1995). Hivyo, lugha hizi zinatumiwa kanisani, misikitini, sokoni, shuleni, siasani na mitaani. Kiswahili pia kimeingia kwenye mawasiliano ya mtandao. Tunachokisisitiza ni kwamba Kiswahili kimepata sura mpya, mbali na kutumiwa katika maeneo yaliyoelekea kutengewa Kiingereza na lugha nyingine za kigeni. Hivi karibuni, Kiswahili kimeanza kufunzwa na kutahiniwa kama somo la lazima nchini Uganda, Libya, Ghana, Burundi na Rwanda. Hali hii imepelekea walimu wengi waliotaalamikia Kiswahili kuhamia maeneo haya ambako wanafundisha Kiswahili kuanzia shule za msingi hadi Vyuo Vikuu.

Bila shaka, huu ni mwanzo mzuri, hasa inapozingatiwa kwamba Kiswahili kimekuwa kikichukuliwa kama lugha ya watu wajanja, wakandamizaji na wajinga (Chiraghdin na Mnyampala, 1977). Nchini Kenya na Tanzania, Kiswahili kimefunzwa katika shule za msingi, za sekondari na hata katika vyuo vikuu vingi: vya kibinafsi na vya kitaifa. Nchini Kenya, kwa mfano, Kiswahili kilianza kutahiniwa kama somo la lazima katika shule za msingi, mnamo 1985. Miaka minne baadaye, yaani 1989, Kiswahili kikatahiniwa kwa mara ya kwanza katika shule za upili, chini ya mfumo wa elimu wa 8:4:4. Ifahamike kwamba vyuo vikuu mbalimbali vya kitaifa, ikiwa ni pamoja na vya kibinafsi nchini Kenya hufunza Kiswahili kama somo.

Vyuo vikuu vya kibinafsi vinavyofundisha Kiswahili kama somo ni pamoja na Daystar, Baraton na Catholic. Katika Chuo Kikuu cha Baraton, wanafunzi wote wanaotoka maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki wanatarajiwa kuchukua somo la Kiswahili ili watosheleze mahitaji ya shahada zao. Somo hilo halichukuliwi hivi hivi, bali wanafunzi hupewa kijitihani cha Kiswahili (Kiswahili placement test) ambacho hulenga katika kupima uwezo na tajriba yao katika lugha ya Kiswahili.

Endapo watadhihirisha upungufu wa aina yoyote katika taaluma ya Kiswahili, basi hupewa kozi za chini zinazosisitiza masuala ya kimsingi ya sarufi ya Kiswahili. Hatua hii imepelekea wanafunzi wengi kujisomea vitabu, magazeti na maandishi ya kimsingi yanayowawezesha kukabiliana na somo hilo la lazima. Pasina shaka, hatua hii imesaidia sio tu katika kukiinua na kukipa hadhi Kiswahili, bali pia imesaidia kukisambaza kotekote barani ambako wahitimu wanatarajiwa kufanya kazi wanaporudi makwao.

Hivi leo, zaidi ya vyuo vikuu mia moja kule Ulaya na Marekani hufunza Kiswahili na baadhi ya lugha za Kiafrika kama somo. Idara za Isimu na Lugha za Kiafrika katika vyuo vikuu vya kitaifa na vya kibinafsi zimechangia harakati hizi za kukikuza Kiswahili, kando na kukifungamanisha na shughuli mbalimbali za kijamii.

Kiswahili kimekuzwa kimaksudi ili kiendelee kutosheleza mahitaji ya kimawasiliano miongoni mwa Watanzania wengi. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (kwa sasa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili -TATAKI) imekuwa katika mstari wa mbele kwenye harakati za kukienzi Kiswahili, mbali na kuzishughulikia lugha kadhaa za Kiafrika zinazotumiwa nchini Tanzania. Taasisi hii imechangia pakubwa katika kukiendeleza Kiswahili na sarufi yake. Taasisi hii huwashirikisha wataalamu wa lugha kutoka vyuo vikuu mbalimbali na mashirika ya aina aina yanayokienzi Kiswahili. Utafiti unaofanywa katika taasisi hii huhifadhiwa katika vitabu na majarida mbalimbali yanayochapishwa humo.

Yafaa tukumbuke kwamba, kote barani Afrika, kuna magazeti mengi yanayochapishwa kwa Kiswahili. Nchini Kenya, kwa mfano, kuna magazeti ya *Taifa Leo*, *Kenya Leo* mbali na yale ya kimaeneo hususan *Nyota ya Mashariki* na *Sauti ya Gusii*. Nchini Tanzania, kuna idadi kubwa ya magazeti yanayoandikwa kwa Kiswahili. Nayo ni kama vile *Uhuru*, *Kasheshe*, *Michezo*, n.k. Pia, kuna idhaa nyingi zinazorusha matangazo yao kwa Kiswahili kote barani. Idhaa hizo pia hurusha vipindi mbalimbali vya Kiswahili. Idhaa hizi zipo katika nchi mbalimbali kama vile Kenya, Uganda, Tanzania, Zanzibar, Burundi, na Afrika Kusini. Katika idhaa hizi, Kiswahili na lugha nyinginezo za Kiafrika hutangazwa kila siku.

Ni kutokana na hali hii halisi ambapo tunaamini kwamba Kiswahili na lugha mbalimbali za Kiafrika zitaendelea kuwepo na kuwatumikia wanajamii kwa miongo mingi ijayo, na pengine, milele, kinyume na mawazo kwamba lugha hizi zitapotea na labda kufa. Ni katika mkabala huu ambapo tunadai kwamba Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika hazitakufa wala kudidimia. Lugha hizi zitaweza kutokomea pale ambapo zitaondolewa kwenye maingiliano ya wanajamii wanaozitumia, hali ambayo, kwa maoni yetu, haitatimia. Hata kama wanaozitumia lugha hizi watapungua kwa kipindi fulani, wengine wengi watazaliwa na kuchukua mahali pao kama watumiaji wa lugha hizo. Tunaamini kwamba nguvu na taratibu za kiutandawazi hazitazimeza lugha za Kiafrika ambazo, kila kukicha, zinasemwa na wenyewe. Matumizi yao ya lugha, kama wanavyodai Njogu na Chimerah (1999) na Chimerah (1998) ni sehemu yao ya maisha.

Lugha za Kiafrika zitaendelea kuhifadhiwa katika mioyo na roho za wanajamii kupitia fasihi simulizi ambayo ipo midomoni, masikioni na akilini mwa wanajamii. Kila siku, fasihi simulizi inajitokeza katika maingiliano kati na baina ya wanajamii na hivyo, hakuna jambo lolote litakalotendeka katika dunia, ambalo limejitenga kabisa na fasihi simulizi. Ni kwa misingi hii ambapo Njogu na Chimera (1999:143) wanadai kuwa:

> Fasihi simulizi inapata kubuniwa kutokana na mazingira ya wanajamii na tabia zao...hivyo tunakuta kuwa tangu kuwepo kwa binadamu ulimwenguni, fasihi hii nayo imekuwepo na imeeleza mambo aina aina katika nyanja mbalimbali za taaluma k.v. lugha, fasihi-andishi, historia, jiografia, falsafa, maadili, elimu na hata sayansi.

Kwa mantiki hii, ndani ya fasihi simulizi, mna maelezo kochokocho kuhusu jinsi binadamu anavvojikimu na kujiendeleza licha ya kupambana na masaibu mbalimbali katika dunia yenye misukosuko na hali zinazotatiza. Fasihi simulizi, ambayo hujitokeza kwenye *ngano,* miviga, mighani, visasili, n.k. hutupa maelezo kuntu kuhusu namna wanadamu kote duniani wanavvoweza kujiepusha na maangamizi kwa kujibunia mbinu bora za kujipatia chakula, makao na elimu.

Mbinu za maingiliano, kupitia fasihi hii, zimemnusuru binadamu hadi leo kando na kumwezesha kuyaboresha maisha yake. Haya yote yako kwenye fasihi simulizi, mama wa taaluma zote. Lugha, kama fasihi simulizi, huwa na lengo la mawasiliano. Hivyo, lugha huwawezesha wanajamii kuingiliana na kutagusana kwa minajili ya kujinufaisha. Labda ni kutokana na hali hii ambapo msomi maarufu, Chinua Achebe, katika miaka ya 1970 na 1980 alidai kwamba fasihi simulizi ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika zilielekea kutishia lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa. Pia alidai kwamba nchi nyingi kote ulimwenguni zinakipa Kiswahili nafasi ya kurushwa hewani kwa wale waliokielewa na kukitumia kama chombo cha mawasiliano. Tutaje hapa kwamba Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ina jopo maalumu linaloshughulikia fasihi simulizi ya Mtanzania katika mapana na marefu yake. Pasina shaka lolote, utafiti uliokwishafanywa katika Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika unabainisha umuhimu wazo katika maisha ya kila siku ya wanajamii husika. Pia, ikumbukwe kwamba Kiswahili, pamoja na baadhi ya lugha za kigeni, zimeweza kuingiliana na kuchukuana vizuri kupitia kamusi za uwili lugha na pia za uwingi lugha. Kamusi hizi, zikiwa pamoja na maandishi mbalimbali yaliyotafsiriwa, huchapishwa katika taasisi hii na katika vyuo na mashirika mbalimbali ya uchapishaji. Nyingi ya kamusi hizi zimetumiwa katika shule na vyuo vingi kote Afrika Mashariki na Kati. Pia, kuna kamusi ya istilahi za utabibu, ya sayansi na teknolojia miongoni mwa nyingine. Nyingi ya kamusi hizi zinatumiwa na wasomaji wa kawaida ambao hutaka kuingiliana na malimwengu yanayochukuliwa kuwa ya wasomi na wataalamu “tukufu”.

Redio na Televisheni, kama vyombo vya habari, navyo vimetekeleza jukumu muhimu la kuzitukuza na kuzienzi lugha za Kiafrika. Nchini Kenya, kwa mfano, kuna stesheni mbalimbali hususan *KBC*, *Kiss FM, Citizen* na *KTN*, ambazo mbali na kutekeleza jukumu muhimu la kuwastarehesha, kuwaelimisha na kuwaburudisha wanajamii, hurusha vipindi vingi vya Kiswahili ambavyo vimejaa mafunzo na maadili yanayoilenga jamii pana. Ieleweke kwamba kutokana na mchango huu, sarufi, msamiati, fasihi-simuizi na vipengele vinginevyo vya lugha hizi za Kiafrika zimewafikia wanajamii ambao wamefaidika pakubwa katika kutagusana na kuingiliana vizuri na wenzao majirani. Kwa kuwa Kiswahili na lugha zingine za Kiafrika ndizo zinaeleweka na kutumiwa na wengi, zitawezaje kulindwa na kuhifadhiwa kama mali na amali ya kizazi hiki na vizazi vingi vijavyo? Hili ni swali litakalojibiwa katika sehemu ifuatayo.

**Maanguko ya Lugha za Kigeni, Maendeleo ya Lugha za Kiafrika**

Kutokana mjadala wetu, pana haja ya kumulika upya nafasi ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika katika maisha ya wanajamii: kijamii, kielimu, kiuchumi na kisiasa. Mjadala wetu haulengi katika kuwahimiza wanajamii watupilie mbali Kiingereza na lugha nyinginezo za Kimagharibi kama lugha za mafunzo; la hasha. Tunacholenga katika makala haya ni uwezekano wa Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika kutumiwa sambamba na lugha za kigeni. Ni kutokana na hatua hii ambapo Kiswahili na lugha hizi zitaweza kujitambulisha kama vyombo muhimu vya mawasiliano shuleni na kwingineko. Kuna wale wanaouliza: Je, hili linawezekana? Katika makala haya, tunasisitiza kwamba serikali za Kiafrika zina jukumu muhimu la kutunga sera madhubuti zinazonuia kuziinua lugha za Kiafrika ili ziwe imara zaidi kama lugha za mafunzo. Katiba ya Kenya (2010) imekitangaza Kiswahili kama lugha rasmi ya kwanza, ambapo Kiingereza ni lugha rasmi ya pili. Hatua hii, kama Msanjila, (2002) anavyodai, ni muhimu kwani itawawezesha wanajamii wengi kushiriki kikamilifu katika shughuli nzima ya kuchangia maendeleo ya nchi kwa kutumia lugha wanayoielewa. Mkabala wetu unajikita kwenye kauli kwamba lugha za kigeni, kwa kiasi kikubwa sana, hudumisha mafunzo shuleni na ni kikwazo kwenye maendeleo ya kitaaluma.

Lugha za kigeni zimeshindwa kuendeleza na kusambaza elimu kwani hazieleweki vizuri na watahiniwa wengi. Kutokana na huku kutokielewa Kiingereza, watahiniwa wengi wameendelea kufeli hasa katika masomo mengine yanayotahiniwa katika darasa la nane na kidato cha nne nchini Kenya. Hali hii, kama tulivyokwishadokeza hapo juu, inatokana na ukweli shakiki kwamba lugha itumikayo katika mafunzo na mitihani haieleweki kwa wanafunzi. Ni kutokana na ukweli huu wa mambo ambapo tunapendekeza kwamba Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika zidumishwe na kutumiwa katika mafunzo ya masomo. Umantiki wa kauli hii upo kwenye ushahidi imara kuwa wanafunzi wengi kote nchini Kenya wanaendelea kuwa na uelewa bora wa lugha hizi wanazotumia tangu utotoni.

Yanayojitokeza katika mengi ya magazeti, japo ni ya kibinafsi, yanaelekea kwenye hitimisho kubalifu kwamba wanafunzi wengi walioufanya mtihani wa kidato cha nne katika mwaka 1989 walifeli kwa wingi kwa sababu hawakuielewa lugha ya Kiingereza ambayo hutumiwa katika kutungia mitihani hiyo. Waandishi wa makala haya tofauti wanaelekea kukubaliana kwamba wanafunzi wengi walishindwa kuyafahamu maagizo yaliyokwenda na maswali mbalimbali katika masomo ya hesabu, sayansi na Kiingereza. Wengi wao walishindwa kuyaelewa mahitaji ya maswali yalivyotolewa, na hivyo, wakaishia katika kutolea majibu yasiyokubalika na yasiyochukuana na maswali yenyewe. Hali hii ilitokana na wanafunzi wenyewe kutozielewa kanuni za kimsingi zinazofungamanishwa na lugha ya Kiingereza. Katika hali hii, pana haja ya serikali ya Kenya kuingilia katika matatizo yanayopelekea kudhoofika kwa elimu nchini Kenya, kwa kuiteua lugha ambayo, pamoja na kwamba inaeleweka kwa wengi, itatumiwa katika kukuza, kuendeleza na kudhibiti utaifa, uzalendo na umoja kote nchini. Sote tunakubaliana kwamba kama watahiniwa wengi hawakielewi Kiingereza, basi watashindwa kuyaelewa yaliyomo, hali inayopelekea kuanguka kwao kwenye mitihani hiyo. Njogu na Chimerah (1999:241) wakiutetea mkabala huu, wanasema:

> Tatizo lililopo ni kwamba nchi nyingi hutumia lugha za kigeni kama lugha rasmi katika kufunzia taaluma za sayansi, teknolojia na siasa. Hivi ni kusema, mwanafunzi hujifunza historia, jiografia, biolojia, hesabu miongoni mwa taaluma nyingine kwa Kiingereza na lugha nyinginezo za kigeni. Taratibu kama hii husambaratisha muundo wa kuwaza…

Wanaoipinga kauli inayotetewa na Chimerah na Njogu hukita mawazo yao katika mantiki kwamba endapo tutazitumia lugha za kienyeji katika kufunzia taaluma mbalimbali, basi tutakuwa tunaelekea kwenye maangamizi makubwa kwani tutashindwa kuingiliana na kutagusana na wenzetu katika ulimwengu unaokwenda mbio na kuchukuana na usasa unaojitokeza kwenye utandawazi. Bila ya shaka, haya ni maoni yaliyopotoka, kama hayakupitwa na wakati. Ukweli ni kwamba mtu yeyote, awe mtafiti, mtaalamu au hata mwananchi ana haki ya kutolea mchango wake kwenye taaluma wanazozielewa kwa kutumia lugha wanazozifahamu vyema.

Kupitia njia ya tafsiri na mtapta, wenzetu walio ng'ambo wanaweza kufikiwa na maarifa, uvumbuzi na tajriba nyinginezo zinazotokana na Waafrika wenyewe. Vilevile, maarifa muhimu yanayotokana na tafiti mbalimbali, yanaweza kuwafikia na kuwanufaisha watu wasiozifahamu lugha hizo za kigeni. Hivyo, taaluma mbalimbali zinahitajika kufunzwa kwa lugha za Kiafrika, hatua kwa hatua na baadaye, mafunzo yote yanayotolewa shuleni yafunzwe kwa lugha hizi. Vivyo hivyo, Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika ziendelee kutumiwa katika taaluma na nyanja mbalimbali za kitaifa mathalani, dini, biashara, siasa bunge na mahakama na katika shughuli nyinginezo za kijamii, kiuchumi nakisiasa. Na, kama Mateere na Kalema (1982) wanavyodai, lugha za kigeni haziwezi kutegemewa katika shughuli

za kusaka maarifa yanayochangia harakati za kimaendeleo katika bara la Afrika. Serikali mbalimbali za Afrika zinahitajika kuchunguza upya sera zao za lugha na pia ziungane katika kuutetea msimamo unaozipendelea lugha za Kiafrika katika shughuli za mafunzo shuleni na vyuoni.

Tanzania kupitia TATAKI imepiga hatua ya mwanzo katika kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zake. Nchi zingine zinahitajika kuungana na Tanzania katika kuzipa hadhi lugha za Kiafrika. Hivyo, kupitia lugha hizi za kigeni, hali za ukengeushi na utabaka huweza kudhihirika bayana katika jamii zetu. Kupitia kwa lugha zetu za Kiafrika, na fasihi simulizi zinazofungamanishwa nazo, wanajamii wataweza kujielewa na pia kuyaelewa malimwengu yao, na hivyo kujithamini. Hivyo, lugha ya mwanajamii ni kivuli, ni kitambulisho chake kisichoweza kufahamika bila ya kurejelea ujumla wa maisha yake.

Uteuzi wa lugha fulani na majukumu yanayofungamanishwa nayo ni masuala ya kimsingi yanayomjeleza mwanajamii, kando na kumhusisha na mazingira yake, ikiwa ni pamoja na ulimwengu mpana. Wanasiasa hawapingi ukweli kwamba Kiswahili kinaweza kuwaunganisha wanajamii, hasa wakiwa katika shughuli mbalimbali za kusaka maendeleo ya kila sampuli. Kwa kweli, lugha hutekeleza jukumu kubwa katika kuwatangamanisha wanajamii ambao wanatarajiwa kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya jamii kwa ujumla. Lugha nyinginezo za Kiafrika nazo zina nafasi nzuri katika jamii kwani hurahisisha mawasiliano ya kimaeneo kupitia njia za redio, televisheni na magazeti yanayoweza kuandikwa katika lugha hizi za kienyeji. Hii ni hatua ambayo inaweza kufikiwa iwapo wananchi walio wengi wataruhusiwa kutumia lugha zao katika kuhifadhi tajriba na maarifa yao.

Kiswahili, sawa na Kigujarati, Kijerumani na Kichina, zitaweza kukidhi mahitaji ya taaluma za sayansi na teknolojia (wa Thiongo, 1986). Lugha, kama kitu kingine chochote kilicho hai, hubadilikabadilika kila uchao. Mabadiliko haya huchangia kukua, kuendelea na kuimarika kwa lugha ambazo hutarajiwa kukidhi mahitaji ya kila aina yanayozuka katika jamii. Hakuna lugha duniani ambayo imefikia kilele cha maendeleo na ambayo imekomaa hivi kwamba haiwezi kuruhusu mabadiliko katika viwango vyake mbalimbali. Kiswahili ni moja katika lugha za Kiafrika ambazo zimepiga hatua muhimu za kimaendeleo, kupitia njia mbalimbali za kukuzia na kuundia msamiati wake, hatua ambayo itaiwezesha lugha hii kumudu na kukabiliana na mahitaji ya kimawasiliano yanayoibuka kila siku.

Katika kuutetea mkabala wetu, waandishi wa makala haya wanapendekeza kwamba nchi za Afrika zinahitaji kuunda taasisi mbalimbali zitakazoshughulikia maendeleo na uhifadhi wa lugha hizi za Kiafrika. Serikali hizi pia zinahitajika kuwa na sera madhubuti kuhusu lugha za Kiafrika. Lugha hizi zinafaa kupewa hadhi na majukumu mbalimbali ili ziendelee kulinda na kuhifadhi mila na tamaduni za wanajamii husika. Nchi za Kiafrika haziwezi kupuuza mila, mali, amali, mirathi na turati za kitaifa, hasa zinavyojitokeza kwenye lugha zinazoeleweka na wengi. Ni kutokana na ukweli huu ambapo kunatokea haja za kuzilinda lugha za Kiafrika.

Katika hali hii, tunafaa kujiuliza: Je, tutafuata hatua gani katika kuzilinda na kuzihifadhi lugha hizi za Kiafrika ili ziendelee kuwatumikia wanajamii? Swali hili litajibiwa katika sehemu inayofuata.

**Kuzienzi Lugha za Kiafrika**

Hatua ya mwanzo katika kuzikuza na kuzipa hadhi lugha za Kiafrika zitaendana na kuwahamasisha wanafasihi waziandikie lugha hizi fasihi za kibunifu. Fasihi hizi, pasina shaka, zitasomwa na wengi na huenda hatua hii ikapelekea lugha za Kiafrika kutambuliwa kwenye ramani ya lugha zilizo muhimu ulimwenguni. Tunaamini kabisa kwamba iwapo hatua madhubuti zitachukuliwa basi huenda lugha hizi za Kiafrika zikapata nafasi nzuri kama lugha za kufundishia katika shule na Vyuo vyetu kote nchini Kenya na barani Afrika. Hivyo, hoja zifuatazo, huenda zikakipa Kiswahili kipaumbele na kitambulisho sahihi kama sehemu halisi ya Mwafrika.

i) Lugha za Kiafrika zinahitajika kuhuishwa. Hapa, pana haja ya kuziandikia kazi mbalimbali za kifasihi.

ii) Waandishi mbalimbali wanahitajika kuzitumia sambamba na lugha zinazosemwa kwamba zimeendelea.

iii) Serikali, mashirika na watu binafsi wanahitajika kufadhili na kuongoza tafiti makinifu katika lugha hizi.

iv) Katika kila nchi ya Kiafrika, kuwe na sera madhubuti inayozitetea na kuhimiza matumizi ya lugha hizi kama lugha za kufundishia katika shule na vyuo vikuu.

v) Kuzipa lugha hizi nafasi katika elimu, biashara na kwenye mawasiliano rasmi na pia yasiyo rasmi.

vi) Kuwaandaa na kuwatayarisha vilivyo wataptaji, wakalimani na watafsiri katika lugha hizi. Hatua hii itawawezesha wataalamu waliobobea nyanja mbalimbali kuingiliana na wanajamii katika masuala yanayohusu maendeleo kwa jumla.

vii) Serikali za Kiafrika ziwe kwenye mstari wa mbele katika kutoa mafunzo kwa lugha hizi za Kiafrika. Walimu watayarishwe vilivyo ili wawe katika nafasi nzuri ya kutoa mafunzo kwa lugha hizi kwa wale watakaohitaji kujifunza lugha hizo.

viii) Idara za lugha, isimu na fasihi zishiriki kikamilifu katika shughuli za kutafiti na kutafsiri kazi za kifasihi za jamii mbalimbali za Kiafrika.

ix) Serikali za Kiafrika, kupitia sheria ya bunge, zitunge sera za lugha zitakazozilinda na kuzihifadhi lugha za Kiafrika.

Mjadala wetu unasisitiza mambo mawili makuu: (i) Lugha za Kiafrika ni chombo muhimu cha kujieleza na (ii) lugha hizi huwawezesha wanajamii wengi kuwasiliana kwa wepesi zaidi. Tumekwishadokeza kuwa lugha, mbali na kwamba ni kitambulisho cha wanajamii, huwapa wanajamii nafasi ya kuyafasiri na kuyaweka wazi maarifa waliyo nayo wanajamii wenye utamaduni ambao unakaribiana kwa kiasi kikubwa. Kwa kutumia lugha hizi, wanajamii-lugha mbalimbali huweza kubadilishana mawazo, tajriba na maarifa yanayolenga katika kukabiliana na changamoto na matatizo mbalimbali yanayowasakama.

Inabainika wazi kwamba tatizo moja ambalo tunahitajika kukabiliana nalo linahusu mielekeo ya baadhi ya wanajamii wenyewe kuhusu lugha za Kiafrika. Kuna wanaoamini kwamba lugha za Kiafrika hazina manufaa yoyote ila huwapotezea wakati na rasilimali ambayo ingetumiwa vinginevyo katika kuleta maendeleo katika jamii. Sharuti tusisitize kwamba lugha zote za kilimwengu ni sawa na zinaweza kukidhi mahitaji ya sayansi na pia yale ya kiteknolojia. Hakuna lugha ya kisayansi kwani lugha hazivumbui wala kugundua chochote. Wataalamu ndio hushiriki katika taratibu za kufanya utafiti wa kitaaluma.

Ubunifu na ugunduzi, bila shaka, upo akilini mwa watu. Waafrika hawashindwi kushiriki kikamilifu katika tafiti za kisayansi kwa sababu lugha zao ni duni, bali ni kwa kuwa ugunduzi waliokwishafanya au watakaoufanya haujatafsiriwa na kuhifadhiwa kwenye vitabu, nyaraka na maandishi mengineyo. Ukweli ni kwamba kuna Waafrika wengi walio na uwezo na maarifa ya kisayansi ila maarifa hayo hayakuhifadhiwa vitabuni. Pale wataalamu hao wanapokufa, basi maarifa na tajriba walizojilimbikizia huzikwa nao.

Manufaa mengine yanayozalishwa na matumizi ya lugha za Kiafrika, hasa katika elimu ni kule kuwaruhusu wanafunzi wengi kuyaelewa yanayofunzwa kwa kutumia lugha wanazozifahamu. Kwa kweli, hali hii huenda ikaimarisha viwango vya elimu na kuiboresha elimu kote barani. Akiifuatilia kauli hii kwa karibu, Okombo (2002) anasema:

> Watu ndio chanzo, washiriki na wanufaikaji wa maendeleo. Ni muhimu kuwashirikisha wanajamii walio wengi kwenye harakati za kimaendeleo. Tunahitajika kuwashirikisha watu kwenye shughuli hizo, kando na kuhakikisha kwamba maendeleo yoyote yanayojiri yanawanufaisha wanajamii hao. Hivyo, wanajamii wanahitajika kutazamwa kama watu huru na wanaoweza kujieleza kwa urahisi. Watu hao pia wachukuliwe kuwa sawa na wenzao, hasa wanapofanya maamuzi yanayohusiana moja kwa moja na maisha yao.

Kuna wale wanaoamini kwamba lugha zilizoko barani ni nyingi na huenda zikatatiza shughuli nzima ya kupata zile chache zinazoweza kumudu mahitaji ya kimafunzo na pia ya kimawasiliano. Ukweli ni kwamba lugha nyingi ni faida na rasilimali ya thamani kubwa. Hali hii inatokana na ukweli kwamba taifa lenye tamaduni nyingi huwa na nafasi nzuri ya kuvuna maarifa na mawazo ya kila namna

kwa kila jamii. Pamoja na kwamba suala hili linaweza kushughulikiwa na taratibu za kisera, yafaa tudokeze kwamba wingi-lugha huibua hisia nyingi za kimabadiliko na pia ni rasilimali nzuri kwa wale wanaotaka kujifunza lugha za wenzao na kufaidi kutokana na tajriba na maarifa ya wenzao.

**Hitimisho**

Makala yamejadili suala kuu la umuhimu wa lugha mbalimbali za Kiafrika kwenye ulimwengu unaoelekea kutawaliwa na nguvu za kiutandawazi. Makala yameonyesha kuwa mataifa mbalimbali ya Kiafrika yanafaa kutunga sera zilizo imara na madhubuti kuhusu lugha, na sera ambazo zitapelekea kuhifadhiwa na kulindwa kwa lugha hizi ili ziwawezeshe wanajamii wengi wanaozielewa, kushiriki katika harakati za kimaendeleo. Lugha hizi, basi, zinahitajika kupandishwa hadhi kwa kutumiwa katika mawasiliano mapana yanayohusu wanajamii wenyewe. Wanajamii wasilazimishwe kutumia lugha wasizozielewa, bali waruhusiwe kushiriki kwenye harakati za kimaendeleo kwa kutumia lugha zisizowakanganya.

**Marejeleo**

Chimerah, R. (1998). *Kiswahili Past, Present and future Horizons*. Nairobi: NUP.

Chiraghdin, S., & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: OUP.

Katiba ya Kenya (2010). Nairobi: Government Printers.

Massamba, D. P. B. (1995). 'Lahaja na Mitindo katika Kiswahili Sanifu' katika Kiango, J. (mh), *Dhima ya Kamusi katika Kusanifisha Lugha*. uk. 1-17.

Mateere, K., & Kalema, J. (1982). *Reconsideration of African Linguistic Policies*. Kampala: OAU Bureau of Languages.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila, Y. P. (2002). "Dhima ya Lugha ya Kiswahili Katika Karne ya Ishirini na Moja" in *Kiswahili Vol. 65.* Dar es Salaam: TUKI

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: JKF.

Okombo, O. D. (2002). 'Language Policy: The Forgotten Parameter in African Development and Governance Strategies'. Inaugral lecture, delivered to the UoN and the Kenya Public.

Senanu, K., & Williams, D. (1995). *Creative Use of Languages in Kenya*. Nairobi: JKF.

TUKI (1983). Lugha ya Kiswahili: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI.

Wa Thiong'o, N. (1986). *Decolonizing The Mind.* Nairobi: Longman.